HEBU TUSHIRIKISHANE IMANI YETU

SHULE YA JUMAPILI YA WATOTO KIMATAIFA

IBADA YA SHULE YA JUMAPILI KIMATAIFA

Kuimba, kusali na kucheza kwa pamoja: watoto duniani kote hufanya ibada. Hadithi za Biblia huwa ni za muhimu sana. Lakini je, watoto wanagundua nini katika Biblia na kitu gani ni cha muhimu kwao? Ni nini kinachowagusa? Kwa kutumia kijitabu hiki watoto duniani kote wanaweza kuambiana kuhusu mambo hayo yanayowagusa na wanayojifunza. Hii ikiwa kama njia ya kukutana, itawawezesha watoto kukuza uelewa wao juu ya watu wanaoishi katika nchi na tamaduni nyingine. Watajifunza kuwa hata kule kutofautiana ni “Utajiri”.

YOU + ME

YOU + ME: FRIENDS AROUND THE WORLD ni mpango wa mafunzo wa sera ya maendeleo kwa watoto wa shule ya Jumapili na shule ya msingi. Watoto kutoka kote duniani watapata kufahamiana katika hali ya usawa (kama marafiki), kiekumeni na kuwa wazi kwa hali zinazofanana na zisizofanana. **YOU + ME: FRIENDS AROUND THE WORLD** ni programu ya missioni ya kiinjili katika mshikamano (Evangelical Mission in Solidarity), ambayo ni umoja wa makanisa na missioni mbalimbali kutoka katika bara la Asia, Afrika, Mashariki ya kati na Ulaya.

Kwa taarifa zaidi tembelea www.ems-friends.org

NA HIVI NDIVYO UNAVYOFANYA KAZI

- katika kijitabu hiki utaona mawazo au mapendekezo kwa ajili ya shule ya watoto ya Jumapili kutoka kitabu cha Marko 9:33:37. Kijitabu hiki kinapatikana pia kwa Kiingereza, Kiindonesia na Kijerumani.
- Tembo aitwaye Emso na ndege mdogo aitwaye Pipit wanafanya ibada pamoja na watoto.
- Watoto wanaweza kuchora mawazo yao juu ya hadithi walizosomewa katika karatasi za kuchorea zinazopatikana katika kijitabu hiki.
- Karatasi zilizochorwa zitatumwa kwa kikundi kingine nje ya nchi.
- Mawasiliano kwa vikundi vya watoto yatafanywa kupitia vikundi rafiki vya mradi wa watu wazima wa kusoma Biblia kwa kutumia macho ya Jamii nyingine. Missioni ya kiinjili katika mshikamano ndiyo inayoendesha mradi huo.
- Kama hushiriki kwenye mradi wa kusoma Biblia wa watu wazima, unaweza pia kutumia urafiki ulionao au uliopo kati yako au yenu na makanisa, miji au watu wa nchi nyingine.

MAPENDEKEZO YA WIMBO

Kutoka kwenye kitabu cha nyimbo za watoto : Mwalimu achague nyimbo au mapambio yanayoendana na somo hili la Marko 9:33-37.

VITENDEA KAZI KWA AJILI YA IBADA YA SHULE YA JUMAPILI

. Kalamu za rangi mbalimbali na karatasi za kuchorea.

. Tembo Emso na ndege Pipit waliondaliwa kwa ubunifu.

. Alama ya upendo (moyo) kwa ajili ya kukalia, kwa mfano iliyokatwa kutoka kwenye boksi au kitambaa.

Makaratasi mengine ya kuchorea unaweza kuyapakua au kuagiza kutoka kwenye tovuti www.ems-friends.org

KWA MUNGU WATOTO WADOGO NI WAKUBWA

MAWAZO KUTOKA KWA MARKO 9:33-37

vipimo vya Mungu sio vya wanadamu, yaani ukubwa, muonekano, cheo, fedha na mamlaka si kitu kwake. kuwahudumia wengine ndio kitu cha muhimu kwa Yesu. Uhudumu maana yake ni kuwepo kwa ajili ya wengine na kusaidiana katika hali mbalimbali za maisha.

Wanaodhaniwa kuwa wadogo katika jamii ni watoto. Yesu anaonyesha jinsi ya kuishi na watoto kwa sababu walio wadogo ni wakubwa mbele za Mungu. Anawatambua walio wadogo na kuonyesha kuwa ni wa thamani. Mbali na hiyo, kuna ahadi ya Mungu ndani yake ya kuwapokea na kuwapenda watoto.

Watoto wanapaswa kujifunza kuwa:
Mimi ni wa thamani na Mungu ananipenda.

HABARI

MIMI NI **EMSO**



HABARI

MIMI NI PIPIT*

*PIPIT NI KIINDONESIA NA MAANA YAKE NI »NDEGE AITWAYE SHOMORO«

friends

WEWE NI WA THAMANI NA MUNGU

HADITHI YA KUFANYA KWA VITENDO

Watoto wakae kwenye mduara.
Ndege mdogo Pipit na yule Tembo Emso wanakutana na kufahamiana kwa mara ya kwanza.

Pipit: *akiwa amejificha kimya chumbani atoe sauti* chwii, chwii, chwii.

Emso: *anawauliza watoto* Je, na ninyi mnasikia sauti hiyo?

Pipit: *kimya kimya..* chwii, chwii, chwii.

Emso: Sauti hii inatokea wapi? Mnaweza kunisaidia kutafuta?
Weka mikono/viganja kwenye masikio kama ishara ya kusikiliza kwa makini.

Pipit: *kimya kimya…* chwii, chwii, chwii.
Watoto wanagundua mahali Pipit alipo.

Emso: Habari! Wewe ni nani?

Pipit: Ninaitwa Pipit.

Emso: Oh, jina hilo linakufaa sana. Mimi ni Emso.

Pipit: *Huku akilialia na kuhema.* Ah sawa....

Emso: Kwani tatizo ni nini, Pipit? Una huzuni!? Inaonekana una majonzi na umejificha chumbani badala ya kukaa na sisi hapa kwenye duara.

Pipit: Ndio, Emso. Ni kweli nina huzuni. Ninapokuangalia wewe na hawa watoto, basi napatwa na huzuni zaidi.

Emso: *Akiwa ameshangazwa sana* Unasema nini? Ninafurahi sana kuwepo hapa na kuwafahamu watoto hawa wote. Na wewe unahuzunika? Kwanini?

Pipit: *akijibu kwa kigugumizi* Si..si..si..ni kwa sababu..... Kwa sababu..... mimi ni mdogo sana. Ninyi wote ni wakubwa kuliko mimi na wewe tembo ni mwenye nguvu sana.

Emso: *Akiwa anamtuliza Pipit* Oh Pipit. Usiwe na huzuni hivyo. Tena! nimekumbuka hadithi moja ya Biblia. Nataka nikuhadithie na utaona jambo la ukubwa tofauti na ulivyofikiri.
Emso anahadithia hadithi kutoka kwenye kitabu cha Marko 9:33-37 kwa maneno yake.



ANAKUPENDA

Yesu alikuwa na marafiki wengi waliokuwa wakiambatana naye. Siku moja walitembea kuelekea mji wa Kapernaum. *Watoto wote watembee kuzunguka duara*. Wakiwa njiani wanafunzi wake waligombana kati yao. Kila mmoja alitaka kuwa mkubwa *kwa kusimama na kujinyoosha*, kuwa mzuri *kwa kupiga makofi*, kuwa mwenye nguvu *kwa kutunisha misuli*, kuwa bora *kwa kuonyesha kidole gumba*, kuwa wa muhimu *kwa kujipangusa mabega* kuliko wengine.

Wanafunzi walitamani kujua, je, Yesu angemtaja nani kuwa ni mkubwa *kwa kusimama na kujinyoosha*, mzuri *kwa kupiga makofi*, mwenye nguvu *kwa kutunisha misuli,* bora *kwa kuonyesha kidole gumba*, wa muhimu *kwa kujipangusa mabega* kuliko wote kati yao. Lakini Yesu alifanya kitu, ambacho wanafunzi wake hawakutarajia hata kidogo.

Alimuita mtoto mdogo akamuweka katikati yao na kumkumbatia *mfanyakazi mmoja aweke alama ya upendo katikati kwa ajili ya kukalia*. Kisha akawaambia: walio wadogo ni wakubwa mbele za Mungu! Kama mkitaka kuwa rafiki zangu, basi muwajali hata wale walio wadogo. Kwa kuwa Mungu anawapenda watoto kwa namna ya pekee.
Kila mtoto anaweza kusimama kwenye alama ya upendo katikati na wote wamwambie „Wewe ni wa thamani na Mungu anakupenda“.

Pipit: Ni Kweli?

Emso: nini?

Pipit: Kwamba walio wadogo ni wakubwa kwa Mungu?

Emso: Ndio.

Pipit: *anafurahi* ..oh, jamani, ni vizuri sana
Pipit anasimama katika alama ya upendo.

KARATASI YA KUCHOREA

Watoto wachore katikati ya alama ya upendo.
. Yesu anamuweka mtoto kati yao. **Mchore Yesu na wewe mwenyewe.**
. Yesu anaona ndani ya kila mtoto kuna kitu cha thamani. **Kitu gani cha thamani kilicho ndani yako? Kichore!**

MSTARI WA KUKUMBUKA

“Mtu akimpokea mtoto mmoja wa namna hii kwa jina langu, anipokea mimi.”
Marko 9:37

MAWASILIANO

Evangelical Mission in Solidarity
YOU+ME: FRIENDS AROUND THE WORLD
Global Learning with children
Vogelsangstr. 62
70197 Stuttgart
Germany

Wahusika
Anna Kallenberger na Annette Schumm
+49 (0) 711 / 636 78 44
info@ems-friends.org
www.ems-friends.org

Evangelical Mission
in Solidarity

IMPRINT **Editors** Anna Kallenberger and Annette Schumm / **Illustrations** Gert Albrecht/
Graphics büro für visuelles, Monika Richter / **Print** RösslerDruck GmbH / 2016 / recycled paper